TAARIFA YA MATOKEO YA MITIHANI YA TAIFA YA KIDATO CHA PILI, DARASA LA SITA NA DARASA LA NNE YA MWAKA 2017, JUMATATU TAREHE 29 JANUARI 2018.

1.0 UTANGULIZI

Ndugu Wazazi, Wanafunzi, Walimu na Wananchi wote na waandishi wa Habari. Ndugu Waandishi wa Habari, leo Jumatatu tarehe 29 Januari 2018, nimewaita ili kuzungumzia kuhusu matokeo ya mitihani ya Taifa ya Darasa la Nne, Darasa la Sita na Kidato cha Pili ya mwaka 2017 ambayo ilifanyika kuanzia tarehe 20/11/2017 na kumalizika tarehe 06/12/2017. Mitihani hiyo ilishirikisha skuli zote za Serikali na za Binafsi. Matokeo ya mitihani hiyo ndio kigezo kinachotumika rasmi kitaifa kwa wanafunzi wa Zanzibar katika ngazi hizo na kila skuli iliyofanya mitihani huu inapaswa kuyatumia matokeo hayo. Kwa mitihani ya Kiadto cha Pili mwaka 2017, kulikuwa na makundi mawili ya watahiniwa wa Kidato cha Pili waliomaliza Elimu ngazi ya Msingi mwaka 2015, Kundi la kwanza walimalizia elimu ya msingi Darasa la Saba (F.II - 7) na kundi la pili walimaliza elimu ya msingi Darasa la Sita (F.II - 6). Wote hawa waliingia Kidato cha 1 pamoja mwaka 2016 na kufanya Mtihani wa pamoja wa Kidato cha Pili mwaka 2017.

Ndugu Wazazi, Walimu, Wanafunzi na Wananchi,

Wanafunzi waliofanya Mtihani wa Kidato cha Pili (6) mwaka 2017 ni wanafunzi walioingia Darasa la Kwanza mwaka 2010 na kumaliza elimu ya msingi ya miaka 6 mwaka 2015 kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya mwaka 2006.

Kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya mwaka 2006, elimu ya lazima kwa wanafunzi wa Zanzibar ni miaka 12, kwa utaratibu wa miaka 2 ya elimu ya maandalizi,

miaka 6 ya msingi na miaka 4 ya elimu ya sekondari hadi Kidato cha Nne. Hivyo, kwa watahiniwa wa Kidato cha Pili wa mwaka 2017, waliomaliza Elimu ya msingi **(kwa miaka sita)** na ambao wamepata alama za jumla za wastani chini ya **Daraja D**, watarudia tena masomo ya kidato cha Pili katika skuli zao na watafanya tena Mtihani wa kidato cha Pili mwaka 2018. Watahiniwa hao waliopata alama za daraja la chini ya D waliosoma Msingi kwa muda wa miaka 6 ni **5,789**. Kufanya hivyo ni utekelezaji wa Sera ya Elimu inayoelekeza wanafunzi wapate elimu ya miaka 12 hadi Kidato cha Nne. Napenda kusisitiza kuwa watakaorudia ni wale tu waliofanya mtihani na kupata alama wastani wa chini wa D na wala sio waliokuwa hawakufanya mtihani kwa sababu ambazo hazikutambulika.

Wanafunzi waliofanya mtihani wa Kidato cha Pili 2017 na kusoma elimu ya msingi kwa miaka 7 ambao wamepata wastani wa alama chini ya D hawatorudia masomo yao kwani wao walifuata mfumo tofauti na huu.

Kwa taarifa hii Walimu Wakuu wanatakiwa kutompokea mwananafunzi anaerudia masomo ambae hayumo kwenye utaratibu ulioelezwa. Pia, napenda kuwajulisha wanafunzi, walimu na wazazi kuwa haki ya kupata elimu hadi kidato cha Nne kwa wanafunzi wa Skuli za sekondari haimaanishi kuwa mwanafunzi ataendelea na masomo bila ya kupimwa na kufaulu. Mwanafunzi atakaepata wastani wa chini atarudia kabla ya kuendelea na masomo yake.

Ndugu Wananchi, Walimu, Wanafunzi na Waandishi wa Habari,

2. KIDATO CHA PILI

2.1. UANDIKISHAJI

Jumla ya watahiniwa **49,515** kutoka Kidato cha Pili (6) na Kidato cha Pili (7) wamesajiliwa kufanya mtihani wa kuingia Kidato cha Pili mwaka 2017 ambao

ni sawa na ongezeko la asilimia **45.42** ikilinganishwa na watahiniwa **27,017** sawa asilimia **52.5** waliofanya mtihani mwaka 2016.

Katika uandikishaji huo, watahiniwa wa kike ni **27,239** sawa na asilimia **55.01** na wa kiume ni **22,276** sawa na asilimia **44.99** waliandikishwa**.** Watahiniwa wa kidato cha Pili (6) ni **22,207** wakiwemo wanawake **12,930** na wanaume **9,277** na kwa watahiniwa wa Kidato cha Pili (7) ni **27,308** wakiwemo wanawake **14,309** na wanaume **12,999**.

2.2 UFANYAJI WA MTIHANI

Jumla ya watahiniwa **46,580** walifanya mtihani wa Kidato cha Pili sawa na asilimia **94.07** ya walioandikishwa wakiwemo wanawake **26,061** sawa na asilimia **55.95** na wanaume **20,519** sawa na asilimia **44.05.**

Kati ya watahiniwa hao, watahiniwa **20,887** ni wa Kidato cha Pili (6) wakiwemo wanawake 1**2,368** na wanaume **8,519** na watahiniwa **25,693** wakiwemo wanawake **13,693** na wanaume **12,000** ni wa Kidato cha Pili (7). Wanafunzi **2,935** hawakufanya mitihani yao.

2.3 MATOKEO YA MTIHANI

Jumla ya watahiniwa **34,458** sawa na asilimia **73.98** ya watahiniwa wote wamefaulu**,** kati yao wanawake ni **20,793** sawa na asilimia **60.34** na wanaume ni **13,665** sawa na asilimia **39.66**. Ufaulu umeongezeka kwa asilimia **3.88** ukilinganisha na watahiniwa **17,581** sawa na asilimia **70.1 k**wa mwaka 2016**.** Watahiniwa **12,122** hawakufaulu wakiwemo **5,789** wa Kidato cha Pili (6) na **6,333** wa Kidato cha Pili (7) sawa na asilimia **26.02.**

Kwa Kidato cha Pili (6) watahiniwa waliofaulu ni **15,098** sawa na asilimia **72.28** wakiwemo wanawake **9,650** sawa na asilimia **46.20** na wanaume **5,448** sawa na asilimia **26.08**. Kwa upande wa Kidato cha pili (7)

watahiniwa waliofaulu ni **19,360** sawa na asilimia **75.35** wakiwemo wanawake **11,143** sawa na asilimia **43.37** na wanaume **8,217** sawa na asilimia **31.98.** Hivyo asilimia ya ufaulu wa watahiniwa wa kike ni mkubwa kuliko wa kiume. Pia, asilimia ya ufaulu wa watahiniwa wa Kidato cha Pili (7) ni mkubwa kwa asilimia **3.07** ukilinganisha na watahiniwa wa Kidato cha Pili (6).

3. DARASA LA SITA

3.1 UANDIKISHAJI

Jumla ya watahiniwa **34,444** waliandikishwa kwa ajili ya kufanya mitihani wa kumalizia elimu ya msingi darasa la Sita mwaka 2017 wakiwemo Wanawake **18,064** sawa na asilimia **52.44** na Wanaume **16,380** sawa na asilimia **47.56.** Hii ni ongezeko la asilimia **3.6** ukilinganisha na watahiniwa wa mwaka 2016 ambao walikuwa ni **33,250.**

3.2 UFANYAJI WA MITIHANI

Jumla ya watahiniwa **32,379** sawa na asilimia **94.0** ya walioandikishwa walifanya mtihani wa darasa la sita wakiwemo wanawake **17,421** sawa na asilimia **53.8** na wanaume **14,958** sawa na asilimia **46.20.**

3.3 MATOKEO YA MTIHANI WA DARASA LA SITA 2017

Jumla ya watahiniwa **31,145** sawa na asilimia **96.19** wamefaulu kuingia Kidato cha Kwanza 2018, kati yao Vipawa ni **138** sawa na asilimia **0.44**. Michepuo ni **1,387** sawa na asilimia **4.45** na wale wanaoendelea na masomo yao katika Sekondari za kawaida ni **29,620** sawa na asilimia **95.11.** Ufaulu huu ni sawa na ongezeko la asilimia **0.99** ukilinganisha na watahiniwa **29,413** sawa na asilimia **95.2** wa mwaka 2016. Aidha watahiniwa **1,234** hawakufaulu mtihani sawa na asilimia **3.81.** Idadi ya watahiniwa waliofaulu vipawa imeongezeka kutoka **71** wa mwaka 2016

hadi **138** kwa mwaka 2017. Pia, idadi ya watahiniwa waliofaulu kuingia michepuo imeongozeka kutoka **889** mwaka 2016 hadi kufikia **1,387** mwaka 2017**.**

4. DARASA LA NNE

4.1 UANDIKISHAJI

Jumla ya watahiniwa **40,206** waliandikishwa kwa ajili ya kufanya mitihani. Kati yao wa kike ni **20,260** sawa na asilimia **50.39** na Wa kiume **19,946** sawa na asilimia **49.61.** Idadi ya watahiniwa imeongezeka kutoka **38,681** mwaka 2016 hadi kufikia **40,206** kwa mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia **3.9**.

4.2 UFANYAJI WA MITIHANI

Jumla ya watahiniwa **37,139** walifanya mtihani wa Darasa la Nne mwaka 2017 sawa na asilimia **92.37** ya walioandikishwa. Kati yao watahiniwa wa kike ni **19,068** sawa na asilimia **51.34** na wa kiume **18,071** sawa na asilimia **48.66**. Wanafunzi **3,067** hawakufanya mtihani sawa na asilimia **7.63** ambao ni pungufu ukilinganisha na watahiniwa **4,015** sawa na asilimia **10.4** kwa mwaka 2016.

4.3 MATOKEO

Jumla ya watahiniwa **26,448** sawa na asilimia **71.21** walifaulu mtihani wao kati yao watahiniwa wa kike **14,764** sawa na asilimia **55.82** na wa kiume **11,684** sawa na asilimia **44.18.** Ufaulu huu ni ongezeko la asilimia **18.11** ukilinganisha na watahiniwa **18,423** sawa na asilimia **53.1** waliofaulu mwaka 2016. Watahiniwa **10,691** sawa na asilimia **28.79** hawakufaulu mtihani. Idadi hii ni ndogo ukilinganisha na watahiniwa **16,258** sawa na asilimia **46.88** kwa mwaka.

5. WANAFUNZI KUMI BORA

KIDATO CHA PILI

Katika mtihani wa Kidato cha Pili mwaka 2017, wanafunzi bora kitaifa ni kama ifuatavyo:

KIDATO CHA PILI (6)

NO	JINA	SKULI	NAM. YA MTIHANI
1.	MARYAM AMOUR JUMA	FIDEL CASTRO	ZS.189/024
2.	MUNDHIR SALIM ALI	FIDEL CASTRO	ZS. 189/051
3.	AHMED KHALFAN ABDALLAH	FIDEL CASTRO	ZS. 189/043
4.	SEIF KHAMIS NASSOR	FIDEL CASTRO	ZS. 189/055
5.	BASWIRA ALI JUMA	FEZA	ZS.232/006
6.	LAYTH NAQUEEB JAWAD	FEZA	ZS.232/032
7.	ANWAR HAIDAR HEMED	FIDEL CASTRO	ZS. 189/044
8.	MUSTAFA KHAMIS SHAABAN	LUMUMBA	ZS.19/048
9.	NADHIFA RAMADHAN SOUD	FIDEL CASTRO	ZS. 189/028
10.	JAMILA IBRAHIIM MOH'D	FIDEL CASTRO	ZS. 189/020

KIDATO CHA PILI (7)

NO	JINA	SKULI	NAM. YA MTIHANI
1.	RAUDHAT ABDALLA MSELLEM	FIDEL CASTRO	ZS.189/028
2.	FIDAUS SALUM SEIF	MAHAD ISTIQAMA	ZS.247/005
3.	RAYA ISSA RAMADHAN	LUMUMBA	ZS. 019/028
4.	FARHAT FEREJ ABDULHABIB	LAUREATE	ZS. 233/012
5.	MARCO ANDREA MASABUDA	MIKINDANI	ZS. 045/038
6.	LUTTFIYYA ABDALLAH SALIM	MAHAD ISTIQAMA	ZS. 247/013
7.	NAJAT WALID KASSIM	LAUREATE INT.	ZS.233/036
8.	SUMAYYA AHMAD YAKOUB	LAUREATE INT.	ZS.233/059
9.	ABDUL-KADIR SALIM HAMAD	FIDEL CASTRO	ZS.189/039
10.	SEIF SELEIMAN SEIF	SUNNI MADRESSA	ZS. 213/074

DARASA LA SITA

Katika mwaka wa masomo wa 2017 wanafunzi bora kwa mtihani wa darasa la sita ni hawa wafuatao:

NO	JINA	SKULI	NAM. YA MTIHANI
1.	MUNIRA RASHID MOH'D	KIJITOUPELE 'A'	ZP.060/125
2.	HAITHAM TAHIR MUSSA	LAUREATE INT. (P)	ZP.384/003
3.	HAITHAM OMAR ABDALLA	MICHAKAINI 'B'	ZP.217/029
4.	HAMID TAHIR MUSSA	LAUREATE INT. (P)	ZP.384/013
5.	KHALFAN MASSOUD SALUM	TUMBE	ZP.195/182
6.	MIKIDADI JUMA ALI	MITIULAYA	ZP.180/175
7.	AYOUB RASHID AHMAD	KIZIMBANI PEMBA	ZP.181/103
8.	HUMOUD MASSOUD FADHIL	LAUREATE INT. (P)	ZP.384/014
9.	ABDUL-MUSAWIR HIJA HAJI	MTONI MSINGI	ZP.054/149
10.	KHADIJA KHAMIS SHEHA	MTOTEPO 'B'	ZP.035/086

DARASA LA NNE

Katika mwaka wa masomo wa 2017 wanafunzi kumi bora ni kama ifuatavyo.

NO	JINA	SKULI	NAM. YA MTIHANI
1.	ARIF SULEIMAN ALLEY	FRANCIS MARIA	ZP.372/065
2.	UMMUKULTHUM JUMA ALI	MITIULAYA	ZP.180/096
3.	SHAIB HAMAD SHAIB	KONDE ISTIQAMA	ZP.285/043
4.	HAJRA NASSOR KHALAIF	GLORIOUS ACADEMY	ZP.342/040
5.	SHAAME NYANGE ALI	P/MCHANGANI	ZP.056/059
6.	ENAAN JOHAN VANDENABEELE	FEZA	ZP.304/023
7.	FADHIL HUSSEIN MWAIBU	MAKADARA	ZP.020/053
8.	FATMA SHAIB ALI	KIZIMBANI PEMBA	ZP.181/020
9.	AISHA RAHIM ALI	MADUNGU MSINGI	ZP.224/006
10.	INTISAAR OMAR HAMAD	JADIDA	ZP.182/070

5.1 SKULI ZENYE WASTANI MKUBWA KITAIFA

Zifuatazo ni skuli zenye wastani mkubwa kitaifa katika Mtihani wa kidato cha Pili.

KIDATO CHA PILI (6)

NO	SKULI NA WILAYA
1.	FIDELCASTRO – CHAKE- CHAKE PEMBA
2.	LUMUMBA – MJINI UNGUJA
3.	MADUNGU 'B' – CHAKE- CHAKE PEMBA
4.	TUMEKUJA – MJINI UNGUJA
5.	BENBELLA – MJINI UNGUJA
6.	MIKUNGUNI – MJINI UNGUJA
7.	KIEMBE SAMAKI 'A' MCHEPUO – MAGHARIBI "B"
8.	MAHAD ISTIQAMA – KATI UNGUJA
9.	ZANZIBAR COMMERCIAL – MAGHARIBI "B"
10.	CHASASA 'B' – WETE PEMBA

KIDATO CHA PILI (7)

NO	SKULI
1.	FIDELCASTRO - CHAKE CHAKE, PEMBA
2.	LUMUMBA – MJINI UNGUJA
3.	S.O.S HERMANN – MAGHARIBI "B" UNGUJA
4.	CHASASA 'B' – WETE,PEMBA
5.	LAUREATE INTERNATIONAL – MAGHARIBI "B" UNGUJA
6.	MAHAD ISTIQAMA – KATI UNGUJA
7.	BENBELLA – MJINI UNGUJA
8.	SUNNI MADRESSA – MJINI UNGUJA
9.	FRANCIS MARIA – MAGHARIBI "B" UNGUJA
10.	J.K.U MTONI – MJINI UNGUJA

NO	SKULI
1.	S.O.S HERMANN – MAGHARIBI "B" UNGUJA
2.	GLORIUS ACADEMY – MJINI UNGUJA
3.	ENGLISH SPEAKING – MJINI, UNGUJA
4.	MAHAD ISTIQAMA – KATI, UNGUJA
5.	ALI KHAMIS CAMP – CHAKE CHAKE PEMBA
6.	LAUREATE INTERNATIONAL – MAGHARIBI "B" UNGUJA
7.	RAUDHA ACADEMY – MAGHARIBI "B" UNGUJA
8.	TRIFONIA ACADEMY – MAGHARIBI "B" UNGUJA
9.	DONGE MSINGI – KASKAZINI "B" UNGUJA
10.	HIGH VIEW INTERNATIONAL – MAGHARIBI "B" UNGUJA

DARASA LA NNE

NO	SKULI
1.	GLORIOUS ACADEMY – MJINI UNGUJA
2.	ALI KHAMIS CAMP – CHAKE CHAKE, PEMBA
3.	FRANCIS MARIA – MAGHARIBI "B" UNGUJA
4.	LAUREATE INTERNATIONAL- MAGHARIBI "B" UNGUJA
5.	MEMON ACADEMY - MJINI , UNGUJA
6.	BILAL ISLAMIC – MJINI, UNGUJA
7.	S.O.S HERMANN – MAGHARIBI "B" UNGUJA
8.	ALHARAMAYN INTENATIONAL – MAGHARIBI "B" UNGUJA
9.	KONDE ISTIQAMA – MICHEWENI, PEMBA
10.	HIGH VIEW INTERNATIONAL – MAGHARIBI "B" UNGUJA

5.2 SKULI ZENYE WASTANI MDOGO KITAIFA

KIDATO CHA PILI (6)

NO	SKULI	WILAYA
1.	KIBENI	Kaskazini "A" Unguja
2.	KIZIMKAZI	Kusini Unguja
3.	MUYUNI	Kusini Unguja
4.	UNGUJA UKUU	Kusini Unguja
5.	UROA	Kusini Unguja
6.	KILINDI	Kusini Pemba
7.	MBUZINI UNGUJA	Magharibi " A" Unguja
8.	MLIMANI MATEMWE	Kaskazini "A" Unguja
9.	JAMBIANI	Kusini Unguja
10.	MWENGE	Magharibi " A" Unguja

KIDATO CHA PILI (7)

NO	SKULI	WASTANI
1.	KISIWA PANZA	Mkoani Pemba
2.	UNGUJA UKUU	Kati, Unguja
3.	MIZINGANI	Mkoani, Pemba
4.	KOMBENI	Magharibi "B" Unguja
5.	KENGEJA	Mkoani, Pemba
6.	GAMBA	Kaskazini "A" Unguja
7.	KIBENI	Kaskazi "A" Unguja

8.	KUSINI	Kusini, Unguja
9.	JAMBIANI	Kusini, Unguja
10.	UROA	Kusini, Unguja

DARASA LA SITA

NO	SKULI	WILAYA
1.	KILOMBERO	Kaskazini "B" Unguja
2.	MTANGANI	Mkoani, Pemba
3.	KIANGA	Magharibi "A" Unguja
4.	HAROUN PEMBA	Micheweni
5.	PETE	Kati, Unguja
6.	SEBLENI	Mjini
7.	MKWAJUNI	Kaskazini A"
8.	UZI	Kati, Unguja
9.	TUMBATU	Kaskazini A, Unguja
10.	BWEFUM	Magharibi "B" Unguja

DARASA LA NNE

NO	SKULI	WILAYA
1.	CHAMBANI	Mkoani, Pemba
2.	MWAMBE	Mkoani, Pemba
3.	MBUYUTENDE	Kaskazini "A" Unguja
4.	KANDWI	Kaskazini "A" Unguja
5.	KILOMBERO	Kaskazini "B" Unguja
6.	KARUME PEMBA	Micheweni, Pemba
7.	UONDWE	Wete, Pemba

8.	NUNGWI	Kaskazini "A" Unguja
9.	TUMBATU	Kaskazini "A" Unguja
10.	MTANGANI	Mkoani, Pemba

6. WATAHINIWA WASIOFANYA MITIHANI

Jumla ya watahiniwa **2,935** wa kidato cha Pili (**1,320** wa Kidato cha Pili (6) na **1,615** wa Kidato cha pili (7). Pia, watahiniwa **2,066** wa Darasa la Sita na **3,068** wa Darasa la Nne hawakufanya mitihani hii. Miongoni mwa sababu za kutofanya mitihani hii ni utoro, ugonjwa, ndoa, uhamisho na kufariki.

KIDATO CHA PILI

SABABU	UTORO	UHAMISHO	UGONJWA	NDOA	KIFO	JUMLA
KIDATO CHA PILI (6)	1,305	2	11		2	**1,320**
KIDATO CHA PILI (7)	1,590	3	16	5	1	**1,615**
JUMLA	**2,895**	**5**	**27**	**5**	**3**	**2,935**

DARASA LA SITA

SABABU	UTORO	UHAMISHO	UGONJWA	NDOA	KIFO	JUMLA
IDADI	2,018	18	27	1	1	**2,065**

DARASA LA NNE

SABABU	UTORO	UHAMISHO	UGONJWA	NDOA	KIFO	JUMLA
IDADI	2,996	48	22	-	2	**3,068**

7. KESI ZA UDANGANYIFU

Kwa mwaka 2017, hakuna kesi ya udanganyifu iliyoripotiwa kwa watahiniwa wa Darasa la Sita na Darasa la Nne. Jumla ya watahiniwa wanane (8) wa Kidato cha Pili walithibitika kufanya udanganyifu kwa kuwa na vipande vya

karatasi vyenye maandishi huku wakifanya mitihani yao. Kitendo ambacho ni kinyume na kanuni za mitihani. Hivyo wanafunzi wote hawa waliothibitika kufanya udanganyifu huo wamefutiwa matokeo yao kwa mujibu wa kanuni ya 58(1) ya Kanuni za Baraza la mitihani la Zanzibar.

Watahiniwa hao ni kutoka Skuli za Fujoni, Mwanakwerekwe "B", Kwa Mtipura na Chuini. Watahaniwa hao ni wenye nambari zifuatazo:-

ZS.74/39/7	**ZS.34/150/7**
ZS.74/33/7	**ZS.34/159/7**
ZS.74/13/7	**ZS.12/512/7**
ZS.34/126/7	**ZS.30/1003/6**

8. MWISHO

Kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tunawapongeza wale wote waliofanikiwa kuendelea na masomo na tunawatakia kila la kheri katika masomo yao. Pia, nawatakia mafanikio mema wanafunzi watakaorudia masomo ya Kidato cha Pili, nataraji kuwa watafanya bidii katika masomo yao ili waweze kupata matokeo mazuri katika mtihani wa marejeo. Aidha, tunawajuilisha wazazi na walimu wakuu kwamba wanafunzi wote wa madarasa ya Nne na Sita ambao hawakufanya mitihani husika kwa sababu zozote zile watalazimika kurudia madarasa hayo na kufanya tena mitihani mwisho wa mwaka 2018.

Kwa wanafunzi wa Kidato cha Pili ambao wamemaliza Kidato cha pili (7) ambao hawakufaulu tunawasihi wasivunjike moyo na tunawashauri Wazazi/Walezi wawapeleke kwenye Vituo vya Kujiendeleza viliopo karibu nao.

Wanafunzi waliofaulu kipawa na michepuo tu ndio watatangazwa kwenye ZBC – Redio. Wanafunzi wa Kidato cha Pili matokeo yao

yatapatikana katika vituo vyao walivyofanyia mitihani au kupitia tovuti ya Wizara ambayo ni **www.moez.go.tz** **.** pia kupitia facebook ya Wizara 'Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali'

Wizara inatoa shukrani za dhati kwa Wazazi, Walimu, na wale wote walioshirikiana nasi katika kufanikisha kazi hii muhimu sana ya Mitihani ya Taifa.

Ahsanteni.